# 1.0 CHAMA CHA USHIRIKA WA AKIBA NA MIKOPO

## 1.1 Maana na Dhana ya SACCOS

Sheria ya Vyama vya Ushirika Na; 20 ya mwaka 2003 inatafasiri SACCOS kuwa ni Chama kilichoandikishwa ambacho malengo yake makuu ni kuhamasisha wanachama wake kujiwekea Akiba na kuwezesha chanzo cha Mikopo kwa wanachama wake kwa kiwango cha Riba cha kadri na kilichokubalika.

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS) ni Asasi ya fedha inayoundwa na watu wanaofahamiana, ambao wamejiunga pamoja kwa hiari yao na ambao wamekubaliana kuweka fedha zao kwa pamoja na kukopeshana kwa lengo la kujiendeleza kiuchumi na kijamii

## 1.2 Historia fupi ya Vyama vya Akiba na Mikopo

Wazo lilianzia kule Ujerumani na mtu aliyeitwa Raiffeisen mnamo mwaka 1847 na baadaye uanzishaji wa SACCOS ulisambaa Ujerumani na nchi nyingine duniani ikiwemo Canada na Italia. Hapa Tanzania, suala la Vyama vya Akiba na Mikopo lilianza katika miaka ya 1960.

## 1.3 Lengo la SACCOS

Madhumuni ya Vyama vya Akiba na Mikopo (SACCOS) ni kuinua hali ya kiuchumi na kijamii ya wanachama wake kwa kuwahimiza wanachama hao kuweka akiba na hivyo kujenga chanzo cha mikopo itakayotolewa kwa wanachama kwa kiwango cha riba cha kadri na kilichokubalika na wanachama wenyewe.

## 1.4 Sheria na Kanuni

Kanuni za Vyama vya Ushirika zimetengenezwa ili kurahisisha utekelezaji wa Sheria Na. 20 ya mwaka 2003. Ili Kanuni ziweze kwenda sambamba na Sheria, zimegawanywa katika sehemu 11 zenye jumla ya Kanuni 127. Miongoni mwa Kanuni hizo, kanuni ya 75 hadi ya 106 zinazungumzia Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS).

Baadhi ya Kanuni hizo zinaelezwa hapa chini.
Kanuni ya 15 inasisitiza majina ya wanachama kuingizwa kwenye Daftari ya Wanachama (Members' Register)

Kanuni ya 75 (3) inazungumzia Mfungamano wa Wanachama (Common Bond). Ni muhimu sana kuangalia mfungamano wa wanaotaka kuanzisha SACCOS au chama kingine chochote cha ushirika kwa kuwa kama hakuna mfungamano wa kudumu, SACCOS itakayoanzishwa inaweza kushindwa kufanya kazi na kudumu.

Kanuni ya 83 inaelezea kuwa Hisa za mwanachama zitarudishwa kupitia Mfuko wa Kukombolea hisa (Share Transfer Fund).

Kanuni ya 88 (1) – (9) inaelezea Taratibu za Uombaji Mkopo, namna Kamati ya Mikopo itakavyochuja Maombi na Dhamana ya Mikopo.

Kanuni ya 89 inaeleza kuwa iwapo uwezo wa kifedha wa chama ni mdogo kuliko maombi ya wanachama, mikopo midogo ndiyo itakayopewa umuhimu wa kwanza.

Kanuni ya 90 inaeleza kuwa kiwango cha juu cha mkopo ni mara tatu ya akiba za mwanachama.

Kanuni ya 92 (1) inaeleza kuwa jumla ya mikopo itakayotolewa na SACCOS kwa wakati wote isizidi robo tatu (3/4) ya Mtaji tete wa SACCOS (Hisa, 20% ya Jumla ya Akiba na Amana, Limbikizo la faida).

Kanuni ya 93 (1) inaeleza kuwa mikopo itatolewa kwa wanachama tu

Kanuni ya 93 (1) inaeleza kuwa hakuna SACCOS itakayoweza kutoa mikopo kwa wasio wanachama isipokuwa kama itaelezwa kwenye Masharti ya SACCOS hiyo na kwa makubaliano na Mrajis kwa masharti atakayoweka ya mtu huyo kuweza kukopeshwa.

Kanuni ya 97 (1) inaeleza kuwa kiwango cha Riba kitapangwa na Mkutano Mkuu na Mkutano Mkuu unaweza kukasimu kwa Bodi kubadilisha kiwango kulingana na hali ya Soko.

Kifungu cha 35 (1) – (3) na Kifungu 36 cha Sheria ya Vyama vya Ushirika ya mwaka 2003 kinazungumzia Haki na Wajibu wa mwanachama katika Chama kama ifuatavyo:

- Hakuna mtu atakayekuwa na haki za uanachama isipokuwa kama amefanya malipo yote yanayopaswa kufanyika ikiwemo kiingilio na hisa
- Hakuna mtu zaidi ya chama kilichoandikishwa, anayeweza kujiunga katika vyama zaidi ya kimoja vyenye shughuli zinazofanana
- Wajibu wa mwanachama katika chama ni wa kikomo cha hisa anazopaswa kulipa
- Kila mwanachama katika chama cha ushirika ana haki ya kura moja

## 1.4 Faida za SACCOS

i). Ukaribu wa huduma
ii). kufahamiana baina ya wanachama
iii). Usalama wa Fedha
iv). Uwezeshaji mikopo kwa riba iliyokubalika na wote
v). Kulipwa faida (katika Akiba au Amana) Kugawiwa Ziada (katika Hisa) baada ya kipindi cha biashara
vi). Wanachama kuelimishwa juu ya:-
   - Matumizi bora ya fedha na mikopo
   - Ujasiriamali
   - Tabia ya kuweka Akiba
   - n.k

## 1.5 Misingi ya Ushirika

Kulingana na Shirikisho la Vyama vya Ushirika Duniani (ICA), Ushirika una misingi yake, nayo ni:-

i) Hiari na Uwazi
ii) Udhibiti wa ki-utawala kidemokrasia
iii) Uhuru wa Kujitawala
iv) Kushirikishwa wanachama ki-uchumi
v) Elimu, Mafunzo na Habari vi) Ushirikiano baina ya Vyama
vii) Kujali maslahi ya Jamii

# 2.0 UANZISHAJI NA USAJILI WA SACCOS

## 2.1 Mambo Muhimu Katika Uanzishaji wa SACCOS

Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo kinaweza kuanzishwa na watu wa aina mbalimbali, vikundi vya uzalishaji mali na/au vya huduma na pia Asasi / Taasisi za kijamii.
Mambo muhimu ya kuzingatia ni:

- nia au haja ya pamoja
- watu wenyewe
- shughuli na miradi ya uchumi
- mahali penyewe
- idadi ya watu

Hata hivyo, utekelezaji wa hatua rasmi za kuanzisha chama unahitaji maelekezo ya Afisa Ushirika wa eneo husika.

## 2.2 Hatua za Uanzishaji na Uandikishaji

Sheria inayosimamia uanzishaji, uendeshaji na uendelezaji wa shughuli za ushirika nchini ni Sheria ya Vyama vya Ushirika Na. 20 ya mwaka 2003. Hivyo, Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo huanzishwa kwa kufuata Sheria hiyo.

Kabla ya chama kusajiliwa kwa mujibu wa sheria, watu wanaotarajia kuanzisha Chama cha Ushirika wa Akiba na Mikopo wanaweza kuchukua hatua za awali kadri watakavyoona inafaa katika kusaidia uundaji wa chama chao. Hatua hizo ni pamoja na:-

- Mikutano ya awali
- Makubaliano ya pamoja

### i) Taarifa/Wito kwa Afisa Ushirika

Baada ya vikundi au wananchi kwa hiari yao wenyewe, kuamua kuanzisha SACCOS watatoa taarifa kwa Afisa Ushirika wa eneo husika ili aje kutoa mwongozo au maelekezo ya uanzishaji wa chama.

## ii) Mkutano Mkuu wa Uanzilishi

Kikundi au wananchi husika watafanya Mkutano wa kuunda chama wakiongozwa na Afisa Ushirika ambaye atakuwa Mwenyekiti wa kikao. Agenda za kikao ni pamoja na:-

- Kutoa ufafanuzi wa nia ya kuanzisha chama.
- ***Kuteuliwa kwa Bodi ya Muda ya Uanzilishi***
- Kutoa ufafanuzi wa taratibu za kazi za wajumbe ili kufanikisha uanzishaji chama husika.
- Kutoa kibali kwa Bodi ya Muda ya Uanzilishi

***Kazi za Bodi ya Muda ya Uanzilishi***

*Bodi hii itafanya maandalizi yote muhimu kulingana na matakwa ya Sheria ya Vyama vya Ushirika. Maandalizi hayo yatajumuisha kazi zifuatazo:-*

- *Kutayarisha Masharti na Sera.*
- *Kutayarisha taarifa ya Uwezo wa Kiuchumi (Kidadisi Uchumi).*
- *Kuandaa Mpango wa Biashara*
- *Kuandaa Makisio ya Mapato na Matumizi*
- *Kuhamasisha wananchi wengi kujiunga, kukusanya viingilio, kupokea fedha za hisa na akiba/ amana.*
- *Kutafuta Ofisi ya chama na kununua vitendea kazi*
- *Kuajiri Mtunza vitabu/ Karani*
- *Kufanya mambo mengine muhimu ya uanzishaji wa chama.*

## iii) Mkutano wa Kujadili Mapendekezo ya Bodi ya Uanzilishi

Baada ya Bodi ya Uanzilishi kukamilisha maandalizi yake, itaitisha mkutano wa wanachama watarajiwa kujadili mapendekezo yaliyotolewa.

## iv) Kuwasilisha Maombi ya Usajili wa Chama

Maombi ya Usajili wa chama yataandaliwa na kuwasilishwa kwa Mrajis Msaidizi kupitia kwa Afisa Ushirika wa Wilaya. Fomu ya maombi ya kuandikishwa chama itafungashwa pamoja na nakala nne za kumbukumbu zifuatazo:-

- Masharti ya Chama
- Makisio ya Mapato na Matumizi
- Taarifa ya Uwezo wa kiuchumi
- Mihtasari ya mikutano miwili ya uanzilishi iliyofanyika
- Ada ya Usajili

Mrajis Msaidizi atapitia maombi ya usajili pamoja na kumbukumbu zinazohusika kwa lengo la kuona kama chama kitarajiwa kina uwezo wa kiuchumi wa kutosha kuendesha shughuli zake na pia kama matakwa mengine ya Sheria yametekelezwa. Akiridhika na maelezo yaliyotolewa atatoa Hati ya Usajili. Asiporidhika ataelekeza marekebisho yanayotakiwa kufanyika

## v) Mkutano Mkuu wa Kwanza

Mkutano Mkuu wa wanachama utaitishwa katika kipindi cha miezi miwili baada ya kupata usajili kwa madhumuni yafuatayo:-

- Chama kukabidhiwa Hati ya Usajili kutoka kwa Afisa Ushirika
- Kupokea Maagizo/ Maelekezo kutoka kwa Mrajis Msaidizi juu ya mambo muhimu ya kuzingatia katika uendeshaji wa chama
- Kujiuzulu kwa Bodi ya Uanzilishi
- Kuchagua Bodi ya Chama
- Kuchagua Kamati ya Usimamizi
- Mkutano huo unaweza pia kuchagua Kamati ya Mikopo au kuacha shughuli hiyo ifanywe na Bodi yenyewe

Utekelezaji wa majukumu ya Bodi na ya Kamati ya Usimamizi utafanywa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Sera, Masharti na Bajeti ya Chama.

# 3.0 UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA SACCOS

## 3.1 Utangulizi

**Masharti ni nini?**
Ni Kabrasha lenye mkusanyiko wa maelezo mbalimbali yanahusu Chama na Wanachama ambayo yanapaswa kufuatwa ili lengo liweze kufikiwa. Ni Dira inayoyongoza ambayo w/chama lazima waifuate.

## 3.2 Masharti ya SACCOS

**Jina na Anwani:** Vinatambulisha SACCOS, wanachama na shughuli zao na eneo la SACCOS yao.

**Madhumuni:** Yanabainisha Lengo la SACCOS na shughuli itakazofanya.

**Uanachama:** Huelezea sifa zote za kujiunga, taratibu za kujiunga na kukoma kwa mwanachama.

**Haki na Wajibu:** Hubainisha mambo muhimu ambayo yakifanyika, SACCOS na Mwanachama zitakuwepo na kuendelea kudumu.

**Mali za SACCOS:** Ni muhimu zitambulike na zile za kudumu zionyeshwe kwenye daftari ya mali kwa tarehe zilipopatikana na thamani yake.

**Taratibu za Akiba, Amana na Mikopo:** Zinaeleza huduma zitolewazo na SACCOS na taratibu zake.

**Uongozi na Usimamizi wa SACCOS:** Mambo yahusuyo Uongozi na Usimamizi ni muhimu sana kwa kuwa Kasoro katika Uongozi na Usimamizi huweza kuua SACCOS

## 3.2 Uongozi wa SACCOS

**Bodi:**
Muda – Miaka 9
Idadi – Wajumbe 5-9
Kazi – Kusimamia shughuli zote za kila siku za SACCOS
Upatikanaji – Kujaza fomu, Kuchuja, Kupiga kura

**Kamati:**
***Usimamizi:*** Kusimamia shughuli na Mali zote za SACCOS
***Mikopo:*** Masuala ya mikopo: Kupokea maombi, Kujadili, Kuamua, Kufuatilia mikopo na kutoa Taarifa

## 3.3 Uendelevu wa Saccos

Uendelevu wa SACCOS unatokana na Uendeshaji na Usimamizi mzuri wa shughuli mbalimbali zifanywazo na SACCOS husika.

### 3.3.1 Mambo yawezeshayo uendelevu wa SACCOS

***a) Uwezo wa Ki-uchumi***

Ni pale SACCOS inapoweza kusimama yenyewe kwa muda mrefu kutokana na Mapato yake (Vyanzo vyake) na sio Fedha za Ufadhili. Aina za uwezo wa kiuchumi ni:-

i) Uwezo wa Kifedha.
ii) Uwezo wa Ki-Taasisi/ Asasi.
iii)

FAHAMU: Kwamba uwezo wa ki-fedha na wa kitaasisi/ asasi kwa pamoja ni muhimu sana ili kuwezesha lengo la kusambaza au kufikisha huduma kwa Idadi kubwa ya watu katika kipindi fulani kufikiwa/ kupatikana.

***b) Kufikia Walengwa***

Ni pale SACCOS inapoweza kufikisha huduma zake kwa watu wengi na huduma zenyewe zikiwa bora (Bidhaa nyingi, Wanachama wengi na zinamudu Ushindani)

*Hali ya kufikia walengwa inaangaliwa kwa kutambua yafuatayo:-*

a) Kina/ Kiwango cha Ufikiaji.
b) Ubora wa Huduma.
c) Ngazi/ Hatua (Scale).

### 3.3.2 Changamoto Zinazoweza Kujitokeza

- Ushindani wa ki-biashara.
- Urasimu mkubwa na Ukiritimba wa Viongozi
- Kugombania uongozi

- Kujenga mazoea na kujisahau kufuata kanuni na taratibu.
- Kujiamini na kujenga dharau.

### 3.3.3 Mambo Yanayoweza Kuzuia/Kukwamisha Uendelevu

Uendelevu wa SACCOS unaweza kukosekana pale Uendeshaji na Usimamizi unapokuwa mbaya kutokana na mambo yafuatayo:-

- Kutokufuatwa kwa Sheria, Kanuni, Masharti, Taratibu na Miongozo mbalimbali iliyowekwa
- Kukosekana kwa Mpango Biashara na Mpango Mkakati
- Kukosekana kwa Bajeti ya Mapato na Matumizi au Bajeti inapokosa kuzingatia hali halisi
- Kukosekana kwa Elimu, Ujuzi/ Uzoefu na Mafunzo ya kuwawezesha Viongozi na Watendaji kufanya kazi zao ipasavyo kwa kuzingatia mabadiliko na ukuaji
- Kuwepo kwa matumizi mabaya ya fedha
- Kutokuwepo kwa utunzaji mzuri wa kumbukumbu
- Mfarakano na Malumbano ya viongozi
- Kujiamini kwa viongozi kupita kiasi
- Kukosekana kwa Uaminifu na Uangalifu
- Kutokuwepo kwa Ushirikishwaji
- Kutokuwepo kwa Ufuatiliaji wa mara kwa mara na Tathmini ili kupima matokeo

# 4.0 UTAWALA BORA

## 4.1 Utangulizi

Katika Ushirika, Utawala Bora ni Utaratibu wa utumiaji madaraka kwa kuwashirikisha wanachama ili kusimamia Raslimali zilizopo katika kuzitumia kwa ajili ya kuinua hali ya maisha ya wanachama hao.

Lengo kuu la kuwashirikisha wanachama ni kutaka kuhakikisha kuwa shughuli za ushirika zinaendeshwa kwa kuzingatia mawazo na maslahi ya wengi, utawala wa sheria, haki , usawa, uwazi na uwajibikaji.

## 4.2 Misingi ya Utawala Bora

Misingi ya tawala bora yakeni:

- DEMOKRASIA
- UTAWALA WA SHERIA
- HAKI NA USAWA
- USHIRIKISHWAJI
- UWAJIBIKAJI na
- UWAZI

## 4.3 Wajibu wa Viongozi katika Demokrasia

a) Kushirikiana na wanachama kulinda Mali za Chama
b) Kuitisha Mikutano kwa mujibu wa Sheria
c) Kutunza vizuri Daftari la wanachama

e) Kuhakikisha kumbukumbu za mahesabu ya chama zinatunzwa vizuri na zinakaguliwa kwa wakati
f) Wanakuwa washauri wazuri wa wanachama kwa maswala yahusuyo mikopo na shughuli zozote za uzalishaji

## 4.4 Wajibu wa wanachama

a) Kushiriki kikamilifu katika shughuli za chama kiuchumi na kijamii
b) Kushiriki kikamilifu katika dhughuli za chaguzi mbalimbali chamani ili kupata viongozi wenye Maadili ya Ushirika
c) Kujielimisha juu ya Sheria ya ushirika, Kanuni na Taratibu zinazotumika kuongoza ushirika
d) Kujenga na kulinda Amani, Mshikamano na Maelewano kwenye ushirika wao.

## 4.5 Sifa za Kiongozi Bora

Ili kuwa na utawala bora ni lazima kuwa na viongozi bora. Kiongozi bora ni yule mwenye sifa zifuatazo:

- Mwezeshaji anayetumia mbinu za mipango shirikishi
- Mwenye uwezo wa kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni na taratibu bila ya upendeleo wa aina yoyote
- Anahakikisha kuwa huduma zinatolewa kwa haki na usawa bila kujali imani na itikadi za watu katika ushirika wao
- Anayehakikisha kuwa uongozi na utawala katika ushirika unalingana na Dhana na Misingi ya Utawala Bora na Demokrasia.

Kila kiongozi wa Chama cha Ushirika anapaswa kuhakikisha kwamba Uongozi na Utawala wa ushirika unafuata Misingi ya Utawala Bora na kwamba mwenendo wake unalingana na sifa za kiongozi bora wa kuchaguliwa na wanachama wenzake kwa kuzingatia sheria ya ushirika ya mwaka 2003.